Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MKOA WA KAGERA
MTIHANI WA UTIMILIFU WA KIMKOA KIDATO CHA NNE, MEI 2020

021 **KISWAHILI**

Muda: Saa 3

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na mbili (12).**
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu C
3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkonomi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa karatasi utakayojibia.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu sahihi katika karatasi yako ya kujibia.

(i) Bainisha tabia ya umbo lililopigiwa mstari katika kitenzi **ib-<u>w</u>-a**
   A. Kaulitendeka
   B. Kaulitendea
   C. Kaulitendeana
   D. Kaulitendwa
   E. Kaulitendesha

(ii) ‘‘Kiti **<u>cha Mfalme</u>** kinaheshimiwa“ katika sentensi hii neno lililopigiwa msitari ni aina gani ya neno katika uainishaji wa maneno?
   A. Kiunganishi
   B. Kihusishi
   C. Nomino
   D. Kiingizi
   E. Kivumishi

(iii) Ipi ni fasili sahihi kuhusu“ Vina“ miongoni mwa fasili zifuatazo?
   A. Msitari wa mwisho wa shairi unaobadilika ubeti mmoja hadi mwingine.
   B. Mistari wa mwisho wa ubeti wa ushairi wenye kujirudia kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.
   C. Idadi ya silabi zinazopatikana katika mstari wa ubeti wa ushairi
   D. Silabi za kati na mwisho za mstari wa ubeti wa shairi zenye mlio unaofanana.
   E. Kifungu cha maneno kinachobeba wazo kuu mojawapo la ushairi.

(iv) Mang’winda <u>amekuwa</u> mtoro sana. Neno lililopigiwa mstari limetumika kama aina ganiya neno?
   A. Kitenzi kikuu
   B. Kiunganishi
   C. Nomino
   D. Kitenzi kisaidizi
   E. Kitenzi kishirikishi

(v) Ipi kati y azifuatazo si sifa ya fasihi simulizi?
   A. Kuwa na hali ya utendaji
   B. Kuonana kwa fanani na hadhira ana kwa ana
   C. Kutopokea mabadiliko ya papo kwa papo
   D. Kuwa kongwe zaidi
   E. Kutolewa kwa njia ya mdomo

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

(vi) Ipi ni maana ya Nahau " Mbiu ya Mgambo" kati ya maana hizi hapa chini:
A. Tangazo maalumu
B. Tia aibu
C. Fanya tashtiti
D. Mluzi wa Mgambo
E. Sare za Mgambo

(vii) Kategoria ya kisarufi inayowakilisha wakati katika kitenzi:
A. Leksimu
B. Kiambishi awali
C. Shina
D. Mtendewa/ Mtendwa
E. Njeo

(viii) Kila lugha duniani inakua kwa kujiongezea msamiati wake, ikiwemo Kiswahili. Kuna njia mbalimbali zinazotumika katika kuunda msamiati wa Kiswahili. Je, unafikiri maneno ***waya, rehema, duka, papai*** ***na korosho*** yamepatikana kwa njia gani kati ya zifuatazo?
A. Kukopa maneno
B. Kutohoa maneno
C. Kuangalia kitu/ Kufananisha umbo
D. Kudondosha maneno
E. Kuambishamaneno

(ix) Dhana mojawapo kati ya hizi huwa na dhima ya kuokoa muda:
A. Ufahamu
B. Fasihi
C. Lughafasaha
D. Masimulizi
E. Hadhithi

(x) Zifuatazo ni tanzu za fasihi simulizi isipokuwa:
A. Ushairi
B. Maigizo
C. Shairi
D. Hadithi
E. Semi

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

2. Oanisha maana za dhana zilizo katika **Orodha A** kwa kuchagua herufi ya dhana husika katika **Orodha B**, kasha andika herufi husika katika karatasi yako ya kujibia.

Orodha A	Orodha B
i. Kueleza jambo kwa maneno machache bila kuipoteza maana yake ya msingi. ii. Alama ya uandishi inayotenga maneno yaliyo katika orodha fulani. iii. Lengo lake kuu huwa ni kujiburudisha tu na si lazima kuwa na vitabu vyote anavyohitaji msomaji kuvisoma. iv. Hutumika katika kukariri maneno yaliyosemwa na mtu mwingine. v. Huhifadhi msamiati, ni chanzo cha tahajia, ni chanzo cha sarufi ya lugha na hutumika katika utafiti hasa wahistoria ya lugha.	A. Ufahamu B. Mkato C. Ufupisho D. Ni aina za ufahamu E. Kamusi F. Lugha fasaha G. Mtajo H. Kusoma kwa burudani

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Weka majina yafuatayo katika ngeli zake:
   a) Ugonjwa
   b) Kipofu
   c) Mchungwa
   d) Uovu

4. Andika methali inayohusiana na mambo yafuatayo:
   (a) Vidole vya binadamu
   (b) Ukulima
   (c) Imani ya binadamu kwa Mungu
   (d) Ulevi

5. (a) Taja njia nne zinazotumika kuunda misimu.
   (b)Misimu huwa na sifa za kuendana na wakati, taja misimu mine iliyozuka kipindi cha serikali ya awamu ya tano nchini Tanzania.

6. Ukuaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili umepitia vipindi vingi tofauti. Fafanua kwa mifano mambo mannne (4) yaliyosaidia kuikuza na kuieneza lugha ya Kiswahili baada yauhuru.

7. Kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya yaTakadini naWatoto wa Mama Ntilie , kwa kifupi ukitumia hoja nne , mbili kutoka kila riwaya, eleza ni jinsi gani mwanaume ameonekana kuwa kikwazo cha maendeleo katika jamii. Tumia mzee Lomolo mo na Mzee Makwati.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

8. Soma kifungu cha habari kifuatacho , kasha jibu maswal iyanayofuata:

Amani. Amani!
Amani huu ndiyo wimbo unaohitajika kusikika masikioni mwa vizazi vyetu vilivyopo lakini na vijavyo. Huu ndiyo ulikuwa wosia alikuwa akiutoa mzee mmoja aitwae Majanga kwa watoto wake. Lakini pia kwa wajukuu zake. Baada ya maneno hayo mjukuu mmoja alimuuliza babu yake, kwanini unapenda tuimbe amani siku zote? Mzee Majanga alisema yafuatayo: Amani ndiyo kila kitu amani huleta umoja na mshikamano, amani huleta maendeleo, amani hufanya watu kulipa hata maduhuli ya serikali, amani huwafanya watu kutunza na kulinda miundombinu mbalimbali, amani huwafanya watu kulala fofofo, amani huwafanya watu kujenga majumba ya kifahari, amani huwafanya watu kula chakula na kushiba, amani inawafanya watu kuongeza familia. Amani ni kila kitu mjukuu wangu.

Baada ya maelezo hayo yote mjukuu wa pili wa mzee Majanga alimuuliza babu yake swali tena. Kwani babu amani kutoweka inasababishwa na nini? Mzee Majanga alimueleza mjukuu wake yafuatayo: kuna vitu na mambo mengi yanayoweza kufanya amani ipotee miongoni mwayo ni pamoja na ufisadi wa viongozi , uongozi mbaya, ukosefu wa haki miongoni mwa watu, matumizi mabaya ya rasimali za nchi, ukabila, vifo vya watu na huduma mbovu kwa wananchi. Punde si punde mjukuu wa tatu aliuliza swali kwa babu yake kuwa kwani amani ikipotea kunatokea madhara gani? Babu alimjibu mjukuu wake kwa kusema kuwa, kwanza usiombe amani hata ya familia ikapotea maana madhara yake huwezi kuyamudu hata siku moja.

Kwanza watu hugeuka na kuwa watumwa nchini mwao. Pili vifo kuongezeka, uharibifu wa miundombinu mfano barabara, reli n.k njaa kali, nchi kumwaga damu, maandamano yasiyoisha, huduma zote za kijamii kuzorota kwa ujumla na hakuna awezaye kufanya lolote lenye tija sehemu ambayo haina amani. Babu alihitimisha wosia wake kwa kuwakumbusha wajukuu zake kuwa wawe mstari wa mbele kuziunga mkono juhudi za mfalme wao anazozifanya ikiwa ni pamoja na kupiga vita rushwa na ufisadi, kujenga uchumi, kujenga aina zote za miundombinu, kuboresha usafiri wa angani na majini lakini kikubwa zaidi kutumia fursa ya elimu bila malipo.
Kabla babu hajakata roho aliwaambia wajukuu zake kuwa “amani ikipotea huwezi kuirudisha kwa urahisi na ni bora njaa ya tumbo kuliko njaa ya akili.”

Maswali

a) Pendekeza kichwa cha habari hii kisichozidi maneno matatu.
b) Unafikiri kwa nini mzee Majanga anahitaji vizazi na vizazi vitunze amani?
c) i) Taja mambo matatu yanaweza kufanya amani itoweke katika nchi.
   ii) Je unahisi amani ikipotea madhara yake huwa ni makubwa sana? Taja mawili tu.
d) Unahisi ni kwa nini mzeee Majanga anaiona njaa ya tumbo ina unafuu kuliko ile ya akili? Toa sababu mbili tu.

SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswa li**matatu (3)**kutoka katika sehemu hii.

9. Wewe ukiwa ni mfanya biashara mashuhuri wa simu kutoka kampuni ya NOKIA, andika tangazo kwa wananchi katika gazeti la Uhuru ili kuwajulisha wateja wako na wananchi kwa ujumla juu ya simu mpya unazozileta msimu wa kiangazi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

ORODHA YA VITABU TEULE KWA SWALI LA 10 – 12

USHAIRI

Wasakatonge	- M.S. Khatibu (DUP)
MalengaWapya	– TAKILUKI (DUP)
MashairiyaChekacheka	– T.A. Mvungi (EP & D.LTD)

RIWAYA

Takadini	– Ben J. Hanson (MBS)
Watotowa Mama Ntilie	– E. Mbogo (H.P)
Joka la Mdimu	– A.J. Safari (HP)

TAMTHILIYA

Orodha	– Steve Raynolds (MA)
NgoswePenziKitovu cha Uzembe	- E. Semzaba (ESC)
KilioChetu	- Medical Aid Foundation

10. “Mshairi siku zote hukemea uonevu katika jamii.” Thibisha kauli hii kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili ulizosoma.

11. “Fasihi ni chuo cha kufundisha maisha kwa jamii husika.” Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya kati ya riwaya mbili ulizosoma.

12. Kwa kutumia hoja tatu kwa kila tamthiliya kutoka katika tamthiliya mbili ulizosoma, jadili kufaulu kwa waandishi katika kipengele cha utumizi wa tamathali za semi.

Search ⇢ www.africona.net